



Muhtasari wa Mwenendo wa Mvua kwa Siku 10 Zilizopita na Matarajio kwa siku 10 Zijazo

**MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA TAREHE 21-30 APRILI, 2021 NA
MATARAJIO YA MVUA KWA TAREHE 01-10 MEI, 2021.**

1.1 MUHTASARI WA MWENENDO WA VIASHIRIA NA MFUMO WA MVUA KWA TAREHE 21-30 APRILI, 2021.

Kati ya tarehe 21-30 mwezi Aprili 2021, migandamizo mikubwa ya hewa iliyo kaskazini mwa dunia (Azores na Siberia) iliendelea kudhoofika wakati ile iliyopo sehemu ya kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) ilii marika. Hli hii ilipelekeea ukanda wa mvua (ITCZ) kusalia katika maeneo ya kaskazini. Joto la bahari katika eneo la kaskazini-mashariki ya Madagaska lilikua la juu ya wastani na hivyo kuleta mchango katika uimarisaji wa kimbunga **Jobo**. Uwepo wa kimbunga karibu na pwani ya nchi yetu pamoja na ukanda wa mvua (ITCZ) ulisaidia kuongeza vipindi vya mvua katika maeneo ya mwambao wa pwani ya nchi yetu. Eneo la kusini-mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola) kuliendelea kuwepo na joto la bahari la wastani hadi juu kidogo ya wastani. Hali hii ilisababisha kupunguza mchango wa mifumo ya kusababisha mvua katika maeneo ya magharibi mwa nchi.

1.2 MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA TAREHE 21-30 APRILI, 2021.

Kwa ujumla, ukanda wa mvua pamoja na uwepo wa kimbunga karibu na pwani ya nchi yetu kulichangia uwepo wa vipindi vya mvua na ngurumo katika maeneo ya pwani na yale ya ukanda wa ziwa Viktoria. Hatahivyo, maeneo ya Magharibi pamoja na kaskazini-mashariki mwa nchi, yalipata vipindi vichache vya mvua zilizoambatana na ngurumo za radi. Maeneo mengine ya nchi yalipata vipindi vichache vya mvua.

2.0 MATARAJIO YA HALI YA HEWA KWA TAREHE 01- 10 MEI, 2021.

2.1 VIASHIRIA NA MFUMO WA MVUA KWA TAREHE 01- 10 MEI, 2021

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) inatarajiwa kuendelea kudhoofika wakati ile iliyopo kusini (St. Helena na Mascarene) inatarajiwa kuendelea kuimarisika. Ukanda wa mvua (ITCZ) unatarajiwa kuendelea kusogea taratibu kuelekeea kaskazini mwa nchi. Upepo unatarajiwa kuvuma kutoka kusini-mashariki hadi Mashariki katika maeneo yote ya pwani ambaa utasababisha kuwepo na vipindi vya mvua hususani katika nusu ya kwanza ya dekadi. Eneo la kusini-mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola) kunatarajiwa kuwa na joto la bahari la wastani hadi juu kidogo ya wastani. Hali hii itapelekeea

Kwa Mawasiliano:

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Ubungo Plaza, Ghorofa ya 3, 388 Morogoro Rd
S. L. P. 3056, 16102 Dar es Salaam, Tanzania. Nukushi: +255 22 2460735, Simu: +255 22 2460706-8
Barua pepe: met@meteo.go.tz, Tovuti: www.meteo.go.tz

kupunguza kasi ya upopo uvumao kutoka magharibi hivyo kupunguza nguvu ya mifumo isababishayo mvua katika maeneo ya magharibi mwa nchi.

2.2 MWELEKEO WA MVUA KWA TAREHE 01- 10 MEI, 2021.

Kanda ya ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara): Vipindi vyta mvua vitakavyoambatana na ngurumo za radi katika baadhi ya maeneo.

Nyanda za juu kaskazini-mashariki (Mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro,): Vipindi vyta mvua vitakavyoambatana na ngurumo za radi katika maeneo machache.

Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba): Vipindi vyta mvua vitakavyoambatana na ngurumo za radi katika baadhi ya maeneo.

Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora): Vipindi vyta mvua zitakazoambatana na ngurumo za radi katika maeneo machache.

Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida): Vipindi vyta mvua nyepesi katika maeneo machache.

Nyanda za juu Kusini-magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa): Vipindi vyta mvua nyepesi katika maeneo machache.

Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi): Vipindi vyta mvua nyepesi katika maeneo machache.

Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma na Maeneo ya kusini mwa Morogoro): Vipindi vyta mvua nyepesi katika maeneo machache.

Imetolewana; **MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA**

Kwa Mawasiliano:

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Ubungo Plaza, Ghorofa ya 3, 388 Morogoro Rd
S. L. P. 3056, 16102 Dar es Salaam, Tanzania. Nukushi: +255 22 2460735, Simu: +255 22 2460706-8
Barua pepe: met@meteo.go.tz, Tovuti: www.meteo.go.tz